JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

# HAIBA NA MICHEZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

## 650 HAIBA NA MICHEZO

Imechapwa na:
Baraza la Mitihani laTanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTIHANI KWA KILA SWALI ........ 2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi ........ 3
2.1.1 Swali la 1: Upimaji na Tathmini katika Somo la Haiba na Michezo ........ 3
2.1.2 Swali la 2: Maandalizi ya Ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo ........ 6
2.1.3 Swali la 3: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo ........ 8
2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo 12
2.1.5 Swali la 5: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia .. 14
2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo ........ 17
2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo ........ 20
2.1.8 Swali la 8: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo 23
2.1.9 Swali la 9: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo ........ 25
2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia ... 28
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha ........ 31
2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia 31
2.2.2 Swali la 12: Misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo ........ 35
2.2.3 Swali la 13: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na Michezo ........ 39
2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo ........ 44
2.2.5 Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo ........ 48
2.2.6 Swali la 16: Upimaji na tathmini katika somo la Haiba na Michezo ........ 53
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ........ 59
4.0 HITIMISHO ........ 59
5.0 MAPENDEKEZO ........ 59
*Kiambatisho A* ........ 60

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A ngazi ya cheti katika somo la Haiba na Michezo. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wakufunzi, wanachuo, watunga sera pamoja na wadau wengine wa elimu. Mtihani ni moja kati ya vigezo vinavyotumika kutathmini mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa hiyo, majibu ya watahiniwa katika mtihani huonesha viwango na ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa waliweza kuyapata katika miaka yao miwili ya mafunzo ya ualimu.

Katika kufanya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri zimeainishwa. Sababu kubwa zilizowafanya watahiniwa wengi kujibu vizuri maswali hayo ni kuelewa matakwa ya maswali, kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutoa ufafanuzi unaotosheleza na kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye maswali.

Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri katika mtihani wa somo la Haiba na Michezo wapo watahiniwa wachache walioshindwa kujibu baadhi ya maswali. Sababu zilizosababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha ni pamoja na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na kutoelewa matakwa ya maswali.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, mrejesho uliotolewa katika taarifa hii utasaidia kuboresha mafunzo ya ualimu kwa ujumla hasa katika somo la Haiba na Michezo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani, watahini, wakufunzi na wote walioshiriki katika maandalizi ya taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja A mwaka 2021 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna watahiniwa walivyojibu mtihani wa somo la Haiba na Michezo.

Maswali ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo yalitokana na mada tano (5) zinazofundishwa katika ngazi ya cheti. Mtihani ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanywa katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyohitaji majibu mafupi. Kila swali lilikuwa na alama 4. Sehemu B ilikuwa na maswali sita (6) ya insha yaliyohitaji majibu marefu. Kila swali lilikuwa na alama 15. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na maswali manne (4) katika sehemu B.

Jumla ya watahiniwa 2,949 sawa na asilimia 100 walifanya mtihani huu. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa ni kizuri kwa sababu watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walifaulu. Madaraja ya ufaulu katika Mtihani wa Ualimu Daraja A huanzia A hadi F kama ifuatavyo: Ufaulu wa Daraja A alama huanzia 80 hadi 100; ufaulu wa daraja B alama huanzia 70 hadi 79; ufaulu wa daraja C alama huanzia 55 hadi 69; ufaulu wa daraja D alama huanzia 40 hadi 54 na ufaulu wa daraja F alama huanzia 0 hadi 39. Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa asilimia 17.46 ya watahiniwa wote walipata daraja A, asilimia 64.62 walipata daraja B, asilimia 17.71 walipata daraja C na asilimia 0.21 walipata daraja D.

Mwaka 2020 jumla ya watahiniwa 3,313 (100%) walifanya mtihani huu. Watahiniwa wote 3,313 (100%) walifaulu mtihani. Hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu kimeendelea kuwa asilimia 100. Jedwali Na. 1 linaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa katika madaraja kati ya mwaka 2020 na mwaka 2021.

| Mwaka | Daraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | F |
| 2021 | 143 | 2,045 | 1,108 | 17 | 0 |
| 2020 | 510 | 1,887 | 517 | 6 | 0 |

**Jedwali Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa Katika Madaraja

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa ufaulu wa kiwango cha daraja A kilikuwa kikubwa zaidi mwaka 2020 (510) kuliko mwaka 2021 (143). Kinyume chake ufaulu wa daraja B umekuwa mkubwa zaidi mwaka 2021(2,045) kuliko mwaka 2020 (1,887). Ufaulu katika kiwango cha daraja C ni mkubwa zaidi mwaka 2021 (1,108) kuliko mwaka 2020 (517). Hata hivyo, ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika miaka yote miwili 2020 na 2021 ni asilimia 100.

Katika kuchambua takwimu za kila swali, makundi matatu (3) ya ufaulu yalitumika, mkundi hayo yanatokana na ukubwa wa alama walizopata watahiniwa katika swali husika. Makundi hayo ni ufaulu hafifu (0-1.5); ufaulu wa wastani (2-2.5) na ufaulu mzuri (3-4) kwa maswali kuanzia la kwanza hadi la kumi. Aidha kuanzia swali la 11 hadi 16, makundi matatu ya alama yalikuwa; 0-5.5, 6-10 na 10.5 - 15. Halikadhalika, makundi ya ufaulu katika kila swali na katika kiambatisho yaliainishwa kwa kutumia rangi ya kijani kuonesha ufaulu mzuri, njano kuonesha ufaulu wa wastani na nyekundu kuonesha ufaulu hafifu. Taarifa hii imeeleza sababu za watahiniwa kujibu vizuri au kutojibu maswali vizuri. Pia sampuli za majibu ya watahiniwa zimewekwa kama vielelezo katika kuonesha mifano halisi ya hoja zilizowasilishwa.

Aidha, taarifa imetoa maoni na mapendekezo yanayoweza kusaidia kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu hususani katika mada zilizokuwa na ufaulu hafifu.

## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTIHANI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inachambua kwa kina ufaulu wa watahiniwa kwa kila swali. Tathmini hii inahusu aina ya maswali, mada zilizotumika katika kutunga maswali, kiwango cha ufaulu katika mada, hitimisho na mapendekezo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zenye ufaulu hafifu.


### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A ilikuwa na jumla ya maswali 10 yenye jumla ya alama 40. Kila swali lilipewa alama 4. Ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii uligawanyika katika makundi matatu kulingana na alama walizopata. Watahiniwa waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walihesabika kuwa na ufaulu mzuri, waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani na waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu. Uchambuzi wa kila swali ni kama ifuatavyo:

#### 2.1.1 Swali la 1: Upimaji na Tathmini katika Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi kazi mbili za tathmini awali na kazi mbili za tathmini endelevu. Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa katika matumizi ya tathmini awali na tathmini endelevu.


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 99.4 ya watahiniwa wote walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa alimia 71.8 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0, asilimia 27.6 walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na asilimia 0.6 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri walielewa matakwa ya swali. Pia walikuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya upimaji na tathmini hususan katika kipengele cha aina za tathmini na kazi zake. Hali hii iliwawezesha kujibu swali hili kwa ufasaha. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza kuwa: *Tathmini awali: hutumika katika kujua maarifa ya awali waliyonayo wanafunzi wanapoanza mpango mpya wa mafunzo. Pia, hutumika katika kubaini matatizo ya wanafunzi katika kujifunza/wanafunzi wenye mahitaji maalum kabla ya mpango wa mafunzo kuanza ili kujua namna ya kuwasaidia. Tathmini endelevu: Hutumika katika kujua maendeleo ya mwanafunzi katika kujifunza kipindi chote cha mafunzo akiwa shuleni pia hutumika katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kubadili njia, mbinu na zana zisizofaa.* Majibu haya ni sahihi na inaonesha watahiniwa walijiandaa vizuri katika mada hii. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri na kukidhi matakwa ya swali.



1. (a) Tathmini awali
(i) Humsaidia mwalimu kujua maarifa ya awali aliyo-nayo mtoto
(ii) Humsaidia mwalimu kujua jinsi ya kumsaidia mtoto katika kujifunza
(b) Tathmini endelevu
(i) Kujua maendeleo ya mtoto katika kujifunza
(ii) Koboresha njia na mbinu za kufundishia


**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alieleza vizuri kazi mbili za tathmini awali na tathmini endelevu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliofaulu kwa kiwango cha wastani (27.6%), baadhi yao walishindwa kukamilisha idadi ya hoja zilizotakiwa katika

kujibu swali. Wengine walitoa hoja za majibu sahihi lakini bila maelezo kama swali linavyotaka. Kwa hiyo, udhaifu huo uliwafanya wapate alama na ufaulu wa wastani kuanzia alama 20. hadi 2.5.

Asilimia 0.6 ya watahiniwa alishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya upimaji na tathmini hususan kazi za tathmini awali na tathmini endelevu. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakulewa vizuri mahitaji ya swali. Mfano wa majibu yasiyosahihi yaliyoelezwa na watahiniwa hao ni kama ifuatavyo: *Tathmini awali ni mchakato wa kutafuta, kuchambua na kutafsiri data ambazo zimepatikana kutokana na upimaji ambapo hufanyika mwanzoni mwa mafunzo fulani na Tathmini endelevu ni aina ya tathmini ambayo hufanyika kipindi chote cha mafunzo fulani kwa kutafuta, kuchambua na kutafsiri data ambazo zimepatikana kwa matokeo ya upimaji.* Majibu hayo ya watahiniwa siyo sahihi kwa sababu wametoa maana ya tathmini awali na tathmini endelevu badala ya kueleza kazi zake. Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 1.


1 Tathmini Awali; Ni aina ya tathmini
ambayo
Kazi za tathmini Awali
i) Kutafuta chanzo cha tathmini
ii) Kuanza na Kutatua tathmini
Kazi za tathmini endelevu
i) Kukusanya data
ii) Kuendeleza tathmini


**Kielelezo Na. 1:2** Sampuli ya Majibu yasiyosahihi katika Swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa alitaja hoja zisizo na mantiki ya maana halisi ya kazi za tathmini awali na tathmini endelevu.

### 2.1.2 Swali la 2: Maandalizi ya Ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha sifa nne za kuzingatia katika kuandaa malengo mahsusi yaliyo bora. Swali lililenga kumpima mtahiniwa kama anajua sifa za malengo mahsusi katika somo la Haiba na Michezo.

Jumla ya watahiniwa wote 2,949 (100%) walifanya swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu watahiniwa (85%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 1. 2.





**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa asilimia 68.0 ya watahiniwa 1849 () walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0; asilimia 17.0 walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na asilimia 15.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Asilimia 68 ya watahiniwa wote walipata kiwango kizuri cha ufaulu. Walipata alama kuanzia 3 hadi 4 kwa sababu walikuwa na ulelewa wa kutosha wa sifa za kuzingatia katika kuandaa malengo mahsusi yaliyo bora. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza kuwa lengo mahsusi katika somo la Haiba na Michezo *lazima liwe mahsusi au wazi, lazima lipimike, lazima*

*liwe na uhalisia, lazima litekelezeke au lifikike na lazima liwe na muda wa kutekeleza.* Majibu haya yaliwafanya wapate alama na ufaulu mzuri katika swali la 2. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.



2. (i) Lengo Mahususi lionashe muda
(ii) Lengo Mahususi lifikike.
(iii) Lengo Mahususi Lipimike
(iv) Lengo Mahususi liwe wazi

**Kielelezo Na. 2.1** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.1; mtahiniwa aliweza kubainisha sifa muhimu nne za kuzingatia katika kuandaa malengo mahsusi yaliyo bora.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 489 (17%) waliofaulu kwa kiwango cha wastani walielewa matakwa ya swali lakini walikuwa na ufahamu wa wastani kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandaa malengo mahsusi yaliyo bora. Watahiniwa hao walitoa hoja chache zisizokidhi matakwa ya swali na wengine walitoa hoja sahihi na zisizo sahihi. Hali hii iliwafanya wapoteze baadhi ya alama na kupata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5.

Aidha, asilimia 15 ya watahiniwa wote walikuwa na ufaulu hafifu kwa sababu walikuwa na ufahamu mdogo wa sifa za malengo mahsusi ya somo la Haiba na Michezo. Watahiniwa walichanganya majibu yao na mambo muhimu ya kuzingatia katika hatua za uwasilishaji wa somo darasani. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza kuwa sifa za kuzingatia katika kuandaa lengo mahsusi lililo bora ni: *lichochee udadisi kwa wanafunzi, kuzingatia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi, kuzingatia uhusiano wa lengo mahsusi na maisha ya kila siku, azingatie urali wa kijinsia, azingatie matumizi ya muda, azingatie matumizi ya mbinu bora, kutumia zana iliyobora na uwepo wa njia bora za upimaji, idadi ya wanafunzi, maudhui ya somo.* Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali la 2.


2. Sifa anazopaswa kuzingatia mwalimu katika kupan-
ya maandalizi ya andalio la somo.
i) Lazima awe na azimio la kazi.
ii) Lazima awe na mwongozo wa ufundishaji
iii) Lazima awe na kitabu cha kiada.
iv) Lazima awe na ratiba ya masomo.


**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa alibainisha sifa za kuzingatiwa na mwalimu katika kuandaa lengo mahsusi lililo bora na badala yake kubainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa maandalio ya somo.

### 2.1.3 Swali la 3: Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 3 lilimtaka mtahiniwa kufafanua hoja nne (4) atakazoandaa na kuziwasilisha kwa walimu wakuu kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Swali hili lililenga kupima mtahiniwa kuhusu matumizi ya misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa haiba na michezo hasa katika kipengele cha umuhimu wa michezo shuleni.


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 96 ya watahiniwa wote walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa watahiniwa 116 (75%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0; watahiniwa 632 (21%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 102 (4%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Chati Na. 3 inaonesha kuwa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri 116 (75%) walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Watahiniwa hao waliweza kufafanua kwa kifupi hoja nne watakazoandaa na kuwasilisha kwa walimu wakuu kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Baadhi ya hoja zilizotolewa na watahiniwa hao ni: *kujenga ukakamavu wa mwili kwa wanafunzi na walimu, kujenga afya njema kwa wanafunzi na walimu ya kutoshambuliwa na magonjwa, kuburudisha na kuelimisha wanafunzi na walimu, kuimarisha amani, umoja, upendo na ushirikiano kati ya wanafunzi na walimu na huibua vipaji mbalimbali, husaidia wanafunzi kuishi maisha ya kufuata sharia, na ni chanzo cha ajira pia.* Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



3. Umuhimu wa michezo katika shule za msingi kwa walimu wakuu:

i) Michezo husaidia kuibua na kukuza kipaji.
- Michezo inasaidia kuibua kipaji alicho nacho mwanafunzi na kuweza kuendeleza.

ii) Michezo husaidia kuimarisha mwili
- Hii kwasababu michezo hutumika kama njia ya mazoezi ambayo mtu akifanya huweza kuimarisha mwili.


iii) Michezo husaidia kujenga ushirikiano na mahusiano mema baina ya watu wao.
- Kati ya walimu na walimu au walimu na wanafunzi kunakuwa na ushirikiano mzuri.

iv) Husaidia kutambulisha shule.
- Michezo hutambulisha shule kutokana na kuwa na wachezaji bora.

**Kilelezo Na. 3.1:** Sampuli ya Majibu sahihi katika Swali la 3

Kwa upande mwingine, asilimia 21 ya watahiniwa waliofaulu kwa kiwango cha wastani walikuwa na ufahamu wa wastani kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Watahiniwa hao waliweza kuorodhesha majibu tu bila kutoa ufafanuzi wowote kama swali lilivyotaka. Baadhi yao waliorodhesha umuhimu huo kuwa ni: *husaidia kujipatia ajira, husaidia kuimarisha afya, husaidia kuimarisha mahusiano na husaidia kujipatia kipato, husaidia wanafunzi kufanya maamuzi ya busara*. Majibu hayo yalisababisha watahiniwa hao wawe na ufaulu hafifu.

Aidha, watahiniwa wachache 102 (4%) walipata ufaulu hafifu kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa mada ya Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa stadi kuhusu umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Aidha, baadhi yao waliorodhesha majibu tu bila ya kufafanua na wengine waliorodhesha hoja zisizo sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua umuhimu wa michezo katika shule za msingi kwa kuwa walivutiwa na maudhui mengine ya somo. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alijibu swali hili kwa kutaja mambo yafuatayo: *maana ya michezo, michezo inayochezwa shule za msingi kwa kuitaja mfano mpira wa miguu, mpira wa pete, michezo ya riadha, umuhimu wa michezo kwa ujumla, umuhimu wa michezo katika shule za msingi*. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa huyo hakuelewa matakwa ya swali kwa sababu ameelezea mpangilio wa mambo atakayowasilisha kwa walimu wakuu badala ya umuhimu wa michezo katika shule za msingi. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 3.


3i. Dhana ya michezo, Ili kuweza kujua maana ya michezo.
ii. Aina za michezo, kuwezesha kujua aina mbalimbali za michezo.
iii. Faida za michezo, Ili kutambua faida tunazozipata katika uchezaji wa michezo.
iv. Hasara za kuto kucheza michezo, Ili kujua madhara tunayoweza kuyapata tusipo cheza michezo.


**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika Swali la 3

Katika kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa aliwasilisha hoja zisizokidhi matakwa ya swali na kushindwa kufafanua hoja hizo kwa ufasaha.

### 2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha hoja nne (4) kwa ufupi kutetea hoja kwamba ufundishaji kiduchu ni kupoteza muda wa wanachuo kujisomea. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia maarifa aliyojifunza kutetea umuhimu wa ufundishaji kiduchu katika kujifunza.

Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla katika swali hili ni mzuri kwa sababu watahiniwa wengi (82%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 4.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa watahiniwa 2,148 (73%) walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0, watahiniwa 273 (9%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na watahiniwa 528 (18%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa wengi (82%) walifaulu swali hili. Hii ni kwa sababu watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri wa mahitaji ya swali na waliweza kubainisha na kutetea hoja kwamba ufundishaji kiduchu ni muhimu. Mifano ya majibu sahihi yaliyowasilishwa na baadhi


ya watahiniwa ni: *Humsaidia mwalimu tarajali kujua jinsi ya kuchambua muhtasari wa somo, kuandaa maazimio ya kazi na maandalio ya somo, kujua zana, njia na mbinu za kufundishia, kujua namna ya kulitawala darasa, kujua mapungufu yake katika ufundishaji, kujiamini anapoenda kufundisha kwa mfano kwenye kituo cha mafunzo kwa vitendo na kujua changamoto atakazokabiliana nazo akiwa kazini.* Hoja hizi zina mantiki inayoendana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa ufasaha.


4. i/ Unasaidia kumjengea ujasiri mwalimu tarajali
ii/ unamsaidia mwalimu tarajali kurekebisha makosa aliyonayo yasijitokeze katika mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo.
iii/ Unamsaidia mwalimu kujua namna ya kutumia muda katika ufundishaji.
iv/ unampa mwalimu tarajali picha halisi na kazi anayosomea.

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3

Kwa upande mwingine asilimia 18 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata ufaulu hafifu. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa baadhi yao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji. Mapungufu hayo yalisababisha watahiniwa hao kushindwa kubainisha na kutetea hoja kuhusu faida za ufundishaji kiduchu kwa wanachuo na hivyo kupata ufaulu hafifu. Mfano wa hoja zilizowasilishwa na baadhi ya watahiniwa hao ni hizi zifuatazo: *Humsaidia mwanafunzi kuhifadhi kumbukumbu kwa muda mrefu, kujipatia muda wa kujisomea, kupata muda wa kupumzisha akili, kupata muda wa kufanya mambo mengine ya ziada, kutochoka ujifunzaji na kukuza ari ya kujifunza, huongeza stadi ya kusoma na kuandika, hongeza ushirikiano baina ya mtu na mtu na husaidia kulifurahia somo.* Hoja hizi zinaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na tafsiri sahihi ya ufundishaji kiduchu. Kutokujua maana sahihi ya ufundishaji kiduchu kulisababisha watahiniwa hao kubainisha majibu yasiyosahihi kwa swali

hili. Kielelezo Na. 4 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali la 4.


4. i. Hukuza na kuibua vipaji
- Hii ina maana kuamba kutokana na michezo husaidia kuibua na kukuza vipaji.

ii. Husaidia kujenga mwili.
- Michezo husaidia kujenga mwili na kufanya mwili usishambuliwe na magonjwa.

iii. Husaidia kukuza Ushirikiano
- Hii pia ina maana kupitia michezo inasaidia kukuza ushirikiano miongoni mwa watu.

iv. Husaidia kupunguza mwili
- Hii ina maana kwamba michezo husaidia katika kupunguza mwili.


**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4, mtahiniwa alitoa na kuelezea kwa kifupi hoja ambazo hazikidhi matakwa ya swali.

### 2.1.5 Swali la 5: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja nne kueleza kwa kifupi umuhimu wa matumizi ya vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Lengo la swali hili lilikuwa kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu umuhimu wa vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 89 ya watahiniwa wote walifaulu. Takwimu hizi za ufaulu wa watahiniwa zimeoneshwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa asilimia 79.0 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0; asilimia 13.0 walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na asilimia 8.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, asilimia 79 ya watahiniwa wote walifaulu swali hili. Sababu za ufaulu huo ni kutokana na watahiniwa hao kuwa na uelewa mzuri kuhusu umuhimu wa vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Hii inatokana na uchambuzi wa vitabu vya ziada walioufanya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa hoja nzuri za baadhi ya watahiniwa ni hizi zifuatazo: *Humsaidia mwalimu kupata maarifa, stadi na ujuzi mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji, humsaidia mwanafunzi kukuza uwezo ya kutafuta na kusoma maandiko mbalimbali yanayomwezesha kukuza uwezo wake wa kufikiri na kutenda, humsaidia mwalimu kujiamini katika ufundishaji wake kwakuwa anakuwa na uhakika na kitu anachokifundisha, humsaidia mwalimu wakati wa kuandaa nukuu za somo kwaajili ya wanafunzi, husaidia kutoa mazoezi mengi kwa mwanafunzi kwaajili ya kumfikirisha mwanafunzi*. Hoja hizi zinaonesha watahiniwa hao wana maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia hususani umuhimu wa vitabu vya ziada. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu vizuri swali la 5.


5. (i) Husaidia kupata maarifa ya ziada juu ya jambo mwalimu alilofundisha hivyo mwanafunzi anaweza kupata maarifa zaidi kwa kutumia kitabu cha ziada

(ii) Hutumika kupata nukuu za kufundishia na kujifunzia pale ambapo mwalimu anakosa kitabu cha kiada na kutumia kitabu cha ziada kupata nukuu za mada husika

(iii) Hutumiwa na mwanafunzi kupata maarifa zaidi ambayo humuwezesha kufahamu mambo mengine mapya na kuyafahamu kabla ya kufundishwa


(iv) Hutumika kama rejea wakati wa kuandaa andalio la somo, kama mwalimu ali kutumia kitabu hicho kupata maarifa ya kuwafundishia wanafunzi

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya Majibu sahihi katika Swali la 5

Kwa upande mwingine, pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali hili, asilimia 13 ya watahiniwa wote walipata ufaulu wa wastani. Hali hii ilisababishwa na baadhi ya watahiniwa kutoa hoja mbili sahihi na hoja mbili zisizo sahihi. Aidha, baadhi ya watahiniwa wwalirudia hoja kwa maneno tofauti. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *"kitabu cha kiada hutumika katika kuongeza maarifa, kitabu cha kiada husaidia kupata maarifa mapya…".*

Aidha, watahiniwa wachache (8%) walipata alama hafifu. Ufaulu huo hafifu ulitokana na baadhi yao kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Hivyo, watahiniwa walishindwa kueleza kwa kifupi umuhimu wa vitabu vya ziada katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mifano wa hoja hafifu zilizotolewa na baadhi ya watahiniwa ni: *Humsaidia mwalimu katika uandaaji wa zana za kufundishia, humsaidia*

*mwalimu katika kuandaa mbinu za ufundishaji, humsaidia mwalimu katika utafutaji wa nukuu za kufundisha, humsaidia mwalimu katika kutunga mtihani, humsaidia mwalimu katika kuandika rejea.* Watahiniwa hawa walikosa maarifa kuhusu stadi za lugha kwa kuandika humsaidia mwalimu badala ya vinamsaidia mwanafunzi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye ufaulu hafifu katika swali la 5.


5. i/ kitabu Cha kiada hutumika kuonesha mpangilio
wa mada zilizopo katika Muhtasari wa Somo
la haiba na michezo.
ii/ kitabu Cha kiada hutumika kuonesha Aina
za Zana za Upimaji zitakazotumika kupima ma
endeleo ya Wanafunzi kitaaluma.
iii/ kitabu Cha kiada hutumika katika kufundi
shwa na kujifunzia darasani kwa ngazi husika.
iv/ kitabu Cha kiada hutumika kuonesha mada
ndogo ya mada kubwa ambayo mafundisho
wa siku husika.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 5


Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa aliweza kutaja na kufafanua hoja ambazo zinakinzana na umuhimu wa vitabu vya ziada katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa akiwa kama mwalimu kubainisha viashiria vinne vinavyoonesha kuwa mwanafunzi ameathirika kutokana na kuishi katika mazingira magumu. Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu viashiria vinavyoonesha kuwa mwanafunzi ameathirika kwa kuishi katika mazingira magumu.

Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ulikuwa mzuri kutokana na watahiniwa 2,853 (97%)

kufaulu kwa kupata alama kuanzia 2.0 hadi 4.0. Takwimu hizi za ufaulu wa watahiniwa zimeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa asilimia 92.0 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0; asilimia 5.0 walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na asilimia 3.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (92%) waliofanya vizuri walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia. Watahiniwa hao waliweza kubainisha viashiria vinavyooonesha mwanafunzi aliyeathiriwa na mazingira magumu anayoishi. Baadhi ya majibu ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa ni haya yafuatayo: *Mwanafunzi kuchelewa shuleni, mwanafunzi kuwa mtoro shuleni na katika vipindi, mwanafunzi kuwa na msongo wa mawazo, mwanafunzi kujitenga na wenzake na mwanafunzi kukosa kujiamini, mwanafunzi kuwa na hasira, mgomvi na lugha chafu, mwanafunzi kuwa mwizi, mwanafunzi kuwa na magonjwa au afya dhaifu, mwanafunzi kukosa mahitaji ya shule kwa mfano sare, viatu, daftari, kalamu na mavazi binafsi; mwanafunzi kushindwa mitihani kwa kiwango kikubwa mfululizo na mwanafunzi kuwa mwasherati na kubeba mimba katika umri mdogo* . Majibu hayo ni sahihi kwa sababu hizo ni baadhi ya tabia za wanafunzi walioathirika kisaikolojia kutokana na kuishi katika mazingira magumu.

Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali la 6 vizuri.

6 (i) Msongo wa mawazo utakao kuwa nao - mwanafunzi

(ii) Kukosa stadi ya ushirikiano na wanafunzi wenzake.

(iii) Kuonyesha tabia mbaya na mienendo isiyofaa kama vile uvutaji wa bangi na ulevi

(iv) Kuwa mtoro wa kudumu katika kuhudhuria masomo shuleni.

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6

Kwa upande mwingine, asilimia 3 ya watahiniwa wote walipata alama hafifu kwa sababu walikosa ufahamu mzuri wa viashiria vinavyoonesha kuwa mwanafunzi anaishi katika mazingira magumu. Watahiniwa hao hawakuelewa vizuri mada ya Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na Michezo hasa katika kipengele cha utambuzi wa haiba za wanafunzi na uhusiano wake katika kujifunza. Mfano wa majibu hafifu ya watahiniwa katika swali hili ni haya yafuatayo: *Mwanafunzi kuwa na aibu, ushiriki katika ujifunzaji wake darasani, maendeleo yake darasani katika kujifunza, tabia aliyonayo, haiba yake, ukaaji wake wa mwili, kutokujua lugha vizuri, tabia na mwenendo, mavazi, ushiriki katika kujifunza, uwezo wa kufanya maamuzi na kufikiri, mwenye upole, kujithamini na kujipenda.* Majibu haya siyo sahihi hayakidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali la 6.

6. (i). Afya Mbaya.

(ii). Lugha.

(iii). Vurugu za Kimaono.

(iv). Ukikivu hafifu.


**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu yasiyokidhi matakwa ya swali la 6

Katika Kielelzo Na. 6.2: mtahiniwa alitaja viashiria kama afya mbaya, usikivu hafifu, lugha na vurugu za kimaono bila ya kutoa ufafanuzi.

### 2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi stadi nne anazotakiwa kuwa nazo mwalimu ili aweze kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia. Kwa hiyo swali lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu stadi za kufaragua zana nzuri katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.


Jumla ya watahiniwa 2,949 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ulikuwa wa wastani kwa asilimia 44.9 japo watahiniwa wengi (55.1% walikuwa na ufaulu hafifu wa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. hafifu kutokana na watahiniwa wengi (55.1%) kupata alama kuanzia 0 hadi 1.15. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7:




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 7: inaonesha kuwa aslimia 55.1 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; asilimia 20.6 walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na asilimia 24.3 walipata alama kuanzia 3 hadi 4.


Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa wengi (55.1%) walipata ufaulu hafifu kwa sababu hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu stadi muhimu kwa mwalimu ili aweze kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kuelewa vema mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na Michezo hasa tofauti kati ya kufaragua zana na kutengeneza zana. Mfano wa majibu ya baadhi ya watahiniwa ni kama ifuatavyo: *Uwezo wa kutengeneza zana inayotarajiwa kutumiwa darasani; uwezo wa mwalimu katika zana anayotarajiwa kutengeneza na kwenda kutumia darasani*; *uwezo wa kuielezea na kuitumia zana inayotarajiwa kutengenezwa na kutumiwa darasani; uwezo wa kuhusianisha zana anayotarajiwa kuitengeneza na mada anayotarajiwa kwenda kuifundishia na kuihusianisha na mazingaira ili aweze kuwasaidia wanafunzi katika kuhusianisha somo na mazingira kupitia zana yake*. Majibu haya siyo sahihi kwa sababu hayakidhi matakwa ya swali. Aidha, uchambuzi wa majibu haya unaonesha kuwa watahiniwa wanakosa stadi ya kujibu maswali mafupi kwakuwa waliandika dondoo tu bila kutoa ufafanuzi ni jinsi gani stadi hizo humsaidia mwalimu kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia. Watahiniwa waliandika dondoo tu ambazo hazina maelezo yoyote. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambayo si sahihi yaliyosababisha apate alama hafifu katika swali la 7.


7. • Stadi ya Ubunifu.
• Stadi ya kujiamini
• Stadi ya uvumilivu.
• Stadi ya udadisi

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 7

Katika Kielelzo Na. 7.2, mtahiniwa aliorodhesha stadi za jumla za maisha katika somo la Haiba na Michezo ambazo husaidia kumjengea mwanafunzi haiba njema na hivyo kutokidhi matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (24.3%) waliokuwa na ufaulu mzuri walielewa vizuri matakwa ya swali. Watahiniwa hao walieleza kwa ufasaha stadi nne anazotakiwa kuwa nazo mwalimu ili aweze kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia. Baadhi ya majibu ya watahiniwa ni haya yafuatayo: *Stadi ya kuchonga: Hii ni stadi ambayo mwalimu atatumia kuchonga vitu mbalimbali kwa mfano mikuki kwa kutumia mti; Stadi ya kuchora: Humwezesha mwalimu kuchora zana za kufundishia somo la Haiba na Michezo kwa mfano kuchora uwanja wa mpira wa miguu, Stadi ya kufinyanga: Ni stadi ambayo mwalimu anaweza kupata zana kwa kufinyanga vitu mbalimbali kwa kutumia udongo wa mfinyanzi na Stadi ya kuunda: Hii ni stadi ambayo humwezesha Mwalimu kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa kuumba maumbo mbalimbali.* Majibu haya ni kielelezo kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu zana za kufundishia na kujifunzia. Kielelezo Na. 7 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri katika swali la 7.


7(i) Stadi za uchorayi mwalimu anaweza kute
ngeneza au kufaragua zana kwa kuchora.

(ii) Stadi ya uandishi, vilevile mwalimu anaweza
kufaragua zana kwa kuandika kwenye kadi
mbalimbali.

(iii) Stadi ya ukataji, pia mwalimu anaweza kufaragu
a zana kwa kukata maumbo mbalimbali mfano
kukata mstatili, maumbo ya mraba kwa
kutumia boksi.

(iv) Stadi ya uchongaji, mwalimu anaweza akafarag
ua zana mbalimbali kwa kutumia stadi ya ucho
ngaji wa maumbo mbalimbali.

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7


Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alieleza vizuri stadi ambazo mwalimu anatakiwa kuwa nazo ili aweze kufaragua zana nzuri za kufundishia na kujifunzia.

Aidha, watahiniwa wachache (20.6%) waliopata ufaulu wa wastani waliwasilisha hoja chache bila ya kuelezea kwa kifupi kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.8 Swali la 8: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilitaka mtahiniwa kufafanua kwa ufupi mambo manne ambayo mwalimu wa Haiba na Michezo anapaswa kuzingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Lengo la swali hili lilikuwa kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu mambo ya kuzingatia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla katika swali hili ni mzuri kwa sababu asilimia 82 ya watahiniwa wote walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.




**Chati Na. 8** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 8:*

Chati Na. 8: inaonesha kuwa asilimia 52 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4; asilimia 30 walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na asilimia 18 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 52% ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walielewa vizuri matakwa ya swali. Watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika kufafanua mambo muhimu ambayo mwalimu anapaswa kuzingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Miongoni mwao waliweza kufafanua kwa ufasaha kwa kutoa mifano kuhusu mambo ya kuzingatiwa na mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya majibu ya watahiniwa ni haya yafuatayo: *Ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia usawa wa jinsia, ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo zaidi, ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia usalama wa wanafunzi na ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia uibuaji wa vipaji vya wanafunzi.* Haya ni majibu sahihi yanayojibu swali la 8 vizuri. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali la 8 kwa ufasaha.


8 Wanapaswa kuzingatia usawa wa jinsia wakati wa uulizaji wa maswali mfano kuuliza swali la kwanza kwa wavulana na swali la pili kwa wasichana

ii) kuzingatia matumizi sahihi ya zana mfano kutumia zana isiyowachosha wanafunzi, bali iwe inawafikirisha wanafunzi.

iii) Kuwashirikisha wanafunzi katika kuwauliza maswali, wakijibu [illegible] kuwasahihisha kama watakuwa wamekosea.

iv) Kuwahusisha wanafunzi katika kufanya mazoezi kwa vitendo mara baada ya kufundisha kinadharia.


**Kielelezo Na. 8:1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi mambo manne ambayo Mwalimu wa somo anapaswa kuzingatia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Kwa upande mwingine, asilimia 30 ya watahiniwa walipata ufaulu wa wastani. Hii ilitokana na baadhi yao kufafanua hoja sahihi chache kinyume

na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine waliorodhesha hoja bila kufafanua, kuwasilisha hoja dhaifu na wengine kukosa kabisa.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu (18%) walikosa ufahamu wa majibu ya swali. Miongoni mwao walioorodhesha hoja bila kufafanua kama swali lilivyotaka. Aidha, wengine walichanganya na mambo ya kuzingatia katika hatua ya uwasilishaji wa somo darasani. Mfano wa majibu ya watahiniwa yasiyosahihi ni haya yafuatayo: *kutoa mifano, kuuliza maswali wanafunzi, kuhusianisha somo na mazingira, matumizi sahihi ya zana za kufundishia, matumizi sahihi ya mbinu za kufundishia na kujifunzia*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa yasiyosahihi katika swali la 8.2.



08. i) Mpangilio mzuri wa darasa
ii) kuwepo kwa uhimizaji baina yake na wanafunzi
iii) kuwepo kwa mtiririko mzuri wa mada
iv) kuwa na maandalizi ya kutosha/ nukuu.


**Katika Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi

Katika kilelezo 8.2, mtahiniwa aliwasilisha hoja zisizokidhi mahitaji ya swali hivyo, kupata lama hafifu.

### 2.1.9 Swali la 9: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuainisha zana nne anazohitaji mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya Azimio la Kazi na kwa kila moja abainishe matumizi yake. Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu aina za zana/nyenzo na matumizi yake katika somo la Haiba na Michezo.


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ni mzuri kwa sababu asilimia 91% ya watahiniwa wote walifaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 4. Ufaulu wa swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 9




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9*

Chati Na. 9: inaonesha kuwa watahiniwa 2,323 (79%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4; watahiniwa 350 (12%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 276 (9%) walipata alama kuanzia 10 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali la 9 unaonesha kuwa asilimia 79 ya watahiniwa wote walikuwa na maarifa ya kutosha katika kuainisha zana nne anazohitaji mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya Azimio la Kazi na matumizi ya kila aina ya zana. Watahiniwa hawa waliweza kuainisha kwa ufasaha zana nne anazohitaji mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya Azimio la Kazi na kwa kila moja kubainisha matumizi yake. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa ni haya yafuatayo: *Muhtasari wa somo: Huonesha mada zinazotakiwa kufundishwa kwa mtiririko mzuri katika ngazi na somo husika; Kalenda ya mwaka: Hutumika kuonesha mihula ya masomo na likizo, Kalenda ya shule: Humsaidia Mwalimu kujua muda wa likizo na matukio mengine shuleni ili kupanga vema muda wa kufundisha; Ratiba kuu ya masomo: Humsaidia mwalimu kugawa vipindi vyake katika maazimio ya kazi, Kiongozi cha Mwalimu: Hutumika kutoa mwongozo wa ufundishaji kwa Mwalimu na Vitabu vya kiada: Hutumika kutoa maarifa na ujuzi wa ziada katika ufundishaji na ujifunzaji*. Majibu haya ni sahihi kwa sababu yanaikidhi haja ya swali la 8. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri katika swali la 9 kwa kutaja aina ya zana na kutoa matumizi yake kwa kifupi.




9a(i) Muhtasari - Kujua idadi ya Mada.
(ii) kalenda ya shule - Kujua siku za Mapumziko
zli kuazimia kulingana na Muda wa Mapunzo
(iii) Kitabu cha kiada - Kujua idadi ya Mada kuanzia
rahisi kwenda ngumu.
(iv) Kiongozi cha Mwalimu - Kufafanua zana na
Mbi'za upimaji na Mbinu za ufundishaji.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.1; mtahiniwa aliyeweza kuainisha aina nne za zana za kuzingatia wakati wa kuandaa Azimio la Kazi na kisha kubainisha matumizi ya kila zana.

Kwa upande mwingine asilimia 12 ya watahiniwa wote waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani. Sababu za kupata ufaulu wa wastani katika swali hili ni kwamba baadhi ya watahiniwa waliainisha majibu sahihi mawili kati ya manne. Aidha, watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa wastani wa mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na Michezo.

Hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa pamoja na kuwa na ufaulu mkubwa wa watahiniwa katika swali hili, asilimia 9% ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu. Sababu kubwa ya ufaulu duni ni watahiniwa kutokuwa na ufahamu wa kutosha katika zana anazohitaji mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya Azimio la Kazi. Baadhi ya watahiniwa walikosa tafsiri sahihi ya neno zana kama lilivyotumika kwenye swali. Hali hii iliwafanya wataje vitu ambavyo havikukidhi mahitaji ya swali na kushindwa kuvielezea. Mfano wa majibu ya watahiniwa yasiyosahihi ni haya yafuatayo: *Uwanja, mpira, filimbi, magazeti, televisheni, michoro mbalimbali na kamba.* Kielelezo Na. 9.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 9 vizuri.



9. i) Kalamu ya wino
Kwa ajiri ya kuandikia wino kwenye manila kadi.
ii) Manila kadi;
kwa ajiri ya kupanga vitu ambavyo vinatakiwa viwepo kwa kutumia wino wa Kalamu.
iii) Rula
Kwa ajiri ya kunyoosha ~~au kupiga~~ mistari au mstari kwenye manila kadi ~~kwa~~
iv) Kalamu ya risasi
kwa ajiri ya kuchorea mistari ya kutenganishia vitu kwenye azimio la kazi la somo la haiba na michezo.


**Kielelezo Na. 9:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 9

Katika Kilelezo Na. 9.2, mtahiniwa aliwasilisha vifaa vya kuchorea na kuandikia Azimio la Kazi badala ya zana ambazo zinaonesha vyanzo vya maarifa na matukio katika kuandaa Azimio la Kazi.

### 2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi vigezo vinne vya kuzingatia wakati wa kuchagua kitabu cha kiada kwaajili ya somo la Haiba na Michezo. Swali hili lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu sifa muhimu za kitabu cha kiada cha somo la Haiba na Michezo


Jumla ya watahiniwa 2,949 (100%) walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu watahiniwa 2,813 (96%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 10*:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa asilimia 80 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3.0 hadi 4.0; asilimia 16 walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 na asilimia 4.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Takwimu hizi zinaonesha kuwa asilimia 80 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata ufaulu mzuri kwa sababu walikuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha na sahihi kuhusu mada ya Maandiko, Vitabu na Zana za kufundishia na Kujifunzia. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa kifupi na ufasaha vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua kitabu cha kiada kwaajili ya somo la Haiba na Michezo. Yafuatayo ni baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa: *Kiendane na maudhui ya muhtasari, kiwe na mtiririko mzuri wa maudhui, kiwe na mazoezi mengi ya kutosha na kiwe na cheti cha ithibati na kitumie lugha rahisi na inayoeleweka*. Majibu haya yanakidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.





**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10

Kwa upande mwingine asilimia 16 ya watahiniwa walipata ufaulu wa wastani kutokana na kuwa na ufahamu wa wastani kuhusu vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua kitabu cha kiada kwaajili ya somo la Haiba na Michezo. Hali hii iliwafanya waweze kutoa hoja sahihi na hoja zisizo sahihi. Aidha, wengine waliweza kuorodhesha hoja sahihi bila kueleza kwa kifupi kama swali linavyotaka. Mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo bila maelezo: *kiwe na utoshelevu wa maudhui, kiwe na mazoezi ya kutosha, kiendane na umri wa walengwa na kiwe na mtiririko mzuri wa mada.* Haya majibu yana dosari kulingana na mahitaji ya swali la 10.

Aidha, asilimia 4 ya watahiniwa wote walipata ufaulu hafifu (4%) kwa sababu walikosa kuelewa mahitaji ya swali. Pia watahiniwa hao walikosa ufahamu wa kutosha kuhusu mada ya Maandiko, Vitabu na zana za Kufundishia na Kujifunzia hasa katika kipengele cha vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua kitabu cha kiada kwaajili ya somo la

Haiba na Michezo. Baadhi ya watahiniwa walichanganya kati ya vigezo vya uchaguzi wa kitabu cha kiada na mambo ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada. Wengine walichanganya na mambo yanayosababisha mabadiliko ya mtaala wa elimu katika nchi. Yafuatayo ni baadhi ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu vizuri swali hili: *idadi ya wanafunzi, kutokana na mahitaji ya shule, kutofautiana na madarasa, kisiwe kigeni kwa wanafunzi, falsafa ya nchi, maoni ya wanajamii, kukua kwa sayansi na teknolojia, ufaulu wa wanafunzi kushuka na kiwe na mada zote zinazotakiwa kufundishwa.* Majibu haya siyo sahihi hivyo hayakidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyosahihi.


10. i) Jina la Chapisho
ii) Mwaka wa uchapisho
iii) Maudhui ya chapisho.
iv) Jina la mchapishaji

**Kilelezo Na. 10.**2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 10

Katika Kilelezo Na. 10.2, mtahiniwa aliwasilisha hoja zisizokidhi mahitaji ya swali. Hali hii imemfanya ashindwe kubainisha hoja hizo kwa ufasaha. Majibu aliyotoa ni mambo ya kuzingatia katika uandishi bora wa rejea.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha


Sehemu B ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo ilikuwa na jumla ya maswali sita na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali manne tu. Jumla ya alama ilikuwa ni 60 ambapo kila swali moja lilikuwa na alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligwanyika makundi matatu ambayo ni ufaulu mzuri kuanzia alama 10.5 hadi 15.0, ufaulu wa wastani kuanzia alama 6 hadi 10 na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 5.5.

### 2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali la 11 lilimtaka mtahiniwa akanushe usemi kwamba, “Muhtasari wa somo ni muhimu kwa walimu wageni lakini siyo kwa walimu wazoefu”

kwa kuonesha madhara matano ya kufundisha bila kuwa na muhtasari wa somo. Swali hili lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu umuhimu wa muhtasari katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Jumla ya watahiniwa 2,762 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ni mzuri kwa sababu watahiniwa (99.9%) walifaulu swali hili kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15 kama Chati Na. 11 inavyoonesha.




***Chati Na. 11:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swalila 11*


Chati Na. 11 inaonesha kuwa watahiniwa 2,681 (97.1%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, watahiniwa 78 (2.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 3 (0.1%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Chati Na. 11 inaonesha kuwa asilimia 97.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu vizuri. Sababu za kupata ufaulu mzuri ni pamoja na watahiniwa kuelewa matakwa ya swali. Pia watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa muhtasari katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, watahiniwa walikuwa mahiri katika kujibu maswali ya insha sambamba na kuzingatia maelekezo ya mtihani. Hii inaonesha kuwa watahiniwa waliweza kuchambua muhtasari wa Haiba na Michezo na kuuelewa vizuri. Hali hiyo iliwawezesha baadhi ya watahiniwa kutetea kwa ufasaha kuhusu umuhimu wa muhtasari wa somo

kwa mwalimu. Mfano wa hoja sahihi ni haya yafuatayo: *Kufundisha nje ya malengo ya somo, kukosa mpangilo mzuri wa mada zinazotakiwa kufundishwa, kukosa mbinu bora za kufundishia na kujifunzia zilizomo kwenye muhtasari, kukwamishwa uandaaji wa maazimio ya kazi, na kukosa ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.* Hoja hizi ni sahihi kwa kuwa ziliendana na matakwa ya swali la 11. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 11.

11 Muhtasari wa somo; Ni Ufupisho wa Maudhui au Mada zote Zinazotarajiwa Kufundishwa katika Kiwango fulani Chaelimu na Kwa walengwa Maalumu na Muda Maalumu. Muhtasari wa somo la haiba na Michezo huonyesha Mada ambazo Mwalimu anatakiwa Kuzifundishwa kwa ngazi Fulani ya Elimu. Kuna Madhara Makubwa Kwa Mwalimu asiyetumia Muhtasari wa Somo. Yafuatayo ni Madhara ya Mwalimu Kutokutumia Muhtasari.

Kushindwa kutambua Maudhui yanayo takiwa Kufundishwa; Mwalimu asipotumia Muhtasari ni vigumu kubaini Maudhui ambayo anatakiwa Kuyafikisha Kwa Wanafunzi Wake. Pia Kushindwa Kubaini Muda ambao anatakiwa Kuyifikisha Maudhui Kwa Wanafunzi wa Somo la Haibana Michezo Mfano Mwalimu kubuni Maada au Maudhui ya Kufundisha hivyo Kupelekea wanafunzi Kutomuelewa Mwalimu na Kulichukia somo la Mwalimu wa haiba na Michezo Kwani Mwalimu atakuwa hafundishi Kwa Ufanisi.




Mwalimu Kufundisha bila Mpangilio
Maalumu wa Maudhui; Pia Mwalimu asipotumia
Muhtasari huweza kufundisha bila kufuata au
Kutokuwa na Mpangilio wa Maada kama zinavy
ooredheshwa katika Muhtasari wa Somo husika
Mfano katika muhtasari Maada zimeweza kupangw
a kwanzia Mada rahisi kuelekea ngumu hivyo
Mwalimu asipotumia Muhtasari atachanganya
Maudhui ya Kufundisha anaweza kuanza
Mada ngumu kuelekea rahisi au kuchanganya
changanya Maudhui hivyo Wanafunzi kushindwa
Kuelewa Mpangilio wa Maudhui.
Hitimisho; Ni muhimu kwa Mwalimu wa somo
la haiba na Michezo kutumia Muhtasari wa som
o katika suala zima la Ufundishaji na ujifunzaji
wa Somo la haiba na Michezo. Faida za kutumia
Muhtasari ni kama vile kumpa mwalimu mbinu
na njia za kufundishia pia kumshauri Mwalimu
Zana za Upimaji kwa Wanafunzi wa somo la
haiba na michezo

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11

Katika Kilelezo Na. 11.1, mtahiniwa aliweza kueleza kwa hoja tano madhara ya mwalimu kufundisha bila kuwa na muhtasari wa somo.
Kwa upande mwingine, watahiniwa 78 (2.8%) walipata ufaulu wa wastani kutokana baadhi yao kutokuwa na stadi za uandishi bora wa majibu ya maswali ya insha. Pia, watahiniwa wengine hawakutoa utangulizi wa swali. Aidha, baadhi ya watahiniwa kuweka hitimisho la swali ambayo haiakisi ujumbe uliomo kwenye hoja za swali. Hii ilitokana na watahiniwa hao kushindwa kueleza kwa ufasaha madhara ya mwalimu kufundisha bila kuwa na muhtasari wa somo.

Aidha, asilimia 0.1ya watahiniwa walipata ufaulu hafifu kwa sababu hawakuelewa mahitaji ya swali. Watahiniwa hawa pia walikuwa na maarifa duni kuhusu umuhimu wa muhtasari wa somo kwa mwalimu mzoefu na mgeni. Pia, baadhi ya watahiniwa walikuwa hawana stadi nzuri za kujibu maswali ya insha. Hivyo, watahiniwa hao walifanya maandalizi duni katika kujifunza mada hii ya Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na zana

za Kufundishia na Kujifunzia. Mfano wa hoja duni za watahiniwa hawa ni: "…*hupelekea mwalimu kushindwa kuandaa andalio la somo, mwalimu huweza kufundisha mada zilizoko ndani ya mtaala…".* Kilelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali la 11:



11. Muhtasari ni muhimu kwa walimu wote wageni na wasiyowageni yaani wazoefu, muhtasari huwaidia sana wakati wa uandaaji wa azimio la kazi.
Yafuatayo ni madhara ya kufundisha bila kuwa na muhtasari wa somo.
Itapelekea mwalimu kutoka nje ya mada hii itamfanya mwalimu ashindwe kufikia lengo alilo kusudia.
Pia itamfanya mwalimu ashindwe kufundisha mada fulani katika muda maalum unaotakiwa. kuhingana na kukosekana na muhtasari wa somo husika.
Pia humfanya mwalimu kushindwa kujua alipoishia katika kipindi kilichopita kutokana na kukosekana kwa muhtasari.
Mwalimu kushindwa kutoa majibu atakayouliziwa na mwanafunzi/wanafunzi kwa sababu ya kukosa mwongozo ya ufundishaji
Mwalimu kufundisha bila ya kuandaa kutokana na kukosekana na baadhi ya vitendea kazi
Kwa kumalizia hayo ndiyo madhara yatokanayo na mwalimu kufundisha bila kuwa na muhtasari wa somo.


**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika Swali la 11

Katika Kielelzo Na. 11.2, mtahiniwa hakuelewa mahitaji ya swali. Hali hii ilisababisha mtahiniwa kushindwa kutoa ufafanuzi wa hoja zake na hivyo kupoteza mantiki ya majibu yake.

### 2.2.2 Swali la 12: Misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo

Swali la 12 lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufasaha mambo matano yanayoweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba za wanafunzi. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kueleza kwa undani mambo yanayoweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba za wanafunzi.

Jumla ya watahiniwa 2,129 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ni mzuri kwa sababu watahiniwa 97% ya waliojibu swali walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa watahiniwa 1,351 (64%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, watahiniwa 712 (33%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 66 (3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Chati Na. 12, inaonesha kuwa asilimia 64% ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu vizuri. Sababu za kupata ufaulu mzuri ni pamoja na watahiniwa kuelewa matakwa ya swali. Pia watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayoweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba za wanafunzi. Hii inaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa waliweza kuchambua vizuri mada ya Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Haiba na Michezo hasa ile Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia haiba. Mfano wa majibu sahihi ni: *athari* za *makundi rika, hali ngumu ya maisha, matumizi ya madawa ya kulevya, utandawazi, balehe na kuvunja ungo, hali duni ya familia, migogoro na ugomvi katika familia, malezi mabovu ya wazazi, na ukatili wa hali mbalimbali (adhabu kali, ukatili wa kijinsia, ubaguzi), msongo wa mawazo, uyatima na kutopewa mahitaji ya msingi (chakula, malazi na mavazi).* Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la 12.

2 Tabia: Ni mwenendo mzima aliokuwa nao katika jamii ambao humuongoza katika maisha. Tabia yaweza kuwa nzuri au mbaya katika jamii lakini Haiba, Ni ile hali ya mtu kujitambua yeye ni nani na anauwezo ~~gani~~ na nikuwa namna gani anaweza kutumia uwezo wake katika jamii inayomzunguka. Yafuatayo ni mambo ambayo yanaweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba ya wanafunzi.

Makundi rika: tabia na haiba ya mwanafunzi huweza kuathiriwa na makundi rika. Hii hutokea pale mwanafunzi mwenye tabia au haiba nzuri anaposhirikiana na mwanafunzi mwenzake mwenye tabia na haiba mbaya huweza kusababisha athari katika mabadiliko ya tabia na haiba za wanafunzi darasani au shuleni. Mfano mwanafunzi mpole anaposhirikiana na mwanafunzi mtukutu na mwizi ni rahisi huyo mwanafunzi mpole kuiga tabia za mwanafunzi mwenzake hivyo itakuwa imeathiri tabia na haiba ya mwenzake.

Malezi ya Wazazi: Pia malezi huweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba ya mwanafunzi kutokana na kwamba mlezi au mzazi kushindwa kumrekebisha mtoto wake pale anapoona tabia ya mtoto wake inabadilika. Mfano mtoto anapojichanganya na makundi mabaya ambayo yanamharibia tabia yake walezi kushindwa kumshauri mtoto wao kuachana na makundi hayo.


Maendeleo ya Sayansi na teknolojia: Kutokana na maendeleo haya huathiri mabadiliko ya tabia za wanafunzi kwa sababu wanafunzi kushindwa kuwasikiliza wazazi na walimu wao na kuanza kujifikiria mambo ambayo yapo nje na masomo. Mfano matumizi mabaya ya simu hivyo mtoto au wanafunzi huathirika tabia na haiba zao kutokana na kwamba mda wa masomo yeye anawaza mwalimu amalize kufundisha akatumie simu na anachokiangalia hakimsaidii bali kinamharibia tabia na haiba yake.


Mazingira; Pia mazingira huweza kuathiri mabadiliko ya wanafunzi kutokana na kwamba kuna mazingira mengine yanakuwa rafiki kwa mwanafunzi na mengine sio rafiki kwa mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la haiba ya michezo. Mfano wanafunzi wanapotoka kimichezo kutembelea labda shule nyingine muda mwingine huweza kuweka hata kambi ya wiki au siku mbili tatu hivyo kutokana na mazingira wanayoyakuta yanaweza kuwaathiri tabia zao na haiba zao kama yatakuwa rafiki kwao au sio rafiki kwao.

**Kielelezo Na. 12.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12

Kwa upande mwingine, watahiniwa 712 (33%) walipata ufaulu wa wastani kutokana na baadhi yao kuorodhesha hoja bila kueleza kwa ufasaha kama swali linavyotaka. Aidha, baadhi yao waliwasilisha na kueleza kwa ufasaha hoja chache tofauti na matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa 66 (3%) walipata ufaulu hafifu. Hii ilitokana na baadhi yao kushindwa kuchambua vizuri Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Haiba na Michezo, hasa Misingi ya Kufundishaia haiba. Mfano wa hoja zisizosahihi katika Swali la 12 ni: *hali ya hewa, mwalimu kutaja maumbile ya mwanafunzi, mwalimu kutomchagua mwanafunzi kujibu maswali.* Watahiniwa wamewasilisha hoja zisizokidhi mahitaji ya swali. Hali hii iliwafanya wapate ufaulu hafifu katika swali la 12.


12. Tabia ni yale matendo mtu ambayo huyatenda kila siku au huo
ne kana au kuto onekana mfano tabia
ya uchoyo, ukatimu, kuheshimu laki
pia wizi, ugomvi na uongo. Mam
bo ambayo yanaweza kubadili tabia ya
mwanafunzi
Mazingira ya nyumbani, kama mwa
nafunzi mazingira ya nyumbani ni mazuri
na yana maadili yanaweza kubadili ta
bia kutoka tabia nzuri kwenda mbaya
au mbaya kwenda nzuri.
Kupendwa na kushirikishwa, kwani
mwanafunzi akijua kuwa hapendwi anaweza
kunyesha tabia mbaya lakini kama ana
weza kushirikishwa anaweza kubadili
ka baada ya kujua kua anathaminiwa
Kumuhusisha katika michezo, hii
inaweza kumbadili mwanafunzi kutoka ka
tika tabia mbaya kwenda kwenye tabia
nzuri na kama hatashirikishwa itamfa
nya aache tabia nzuri ashike tabia za
kishamba mbaya.



Uhusiano wa Mwalimu na Mwanafunzi. Endapo uhusiano wao kati ya Mwalimu na Mwanafunzi uko vizuri unaweza kubadili tabia na haiba ya Mwanafunzi kutoka kwenye ubaya kwenda kwenye uzuri au kinyume chake.
Kupewa nafasi ya kuongoza wato [illegible]
Uongozi ili wawe kubadilike. lakini wakiwa sio viongozi huweza kubadili tabia zao
Hiyo mwanafunzi huweza kubadili tabia na haiba yake kutokana na makri ya jamii mazingira mwingika na kuonekana bora kabisa.


**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 12

Katika kielelezo Na. 12.2 mtahiniwa alishindwa kueleza kwa ufasaha mambo matano yanayoweza kuathiri mabadiliko ya tabia na haiba za wanafunzi.

### 2.2.3 Swali la 13: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kwa kutumia hoja tano kufafanua mambo ya kuzingatia ili kuhakikisha usalama wa mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Swali hili lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu usalama wa mwanafunzi wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Jumla ya watahiniwa 1,092 (100%) walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 81.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.





**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 13*

Chati Na. 12: inaonesha kuwa ailimia 35 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, asilimia 46 walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na asilimia 19 walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Chati Na. 12 inaonesha kuwa asilimia 35 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walitambua matakwa ya swali. Hali hii iliwawezesha kufafanua vizuri mambo ya kuzingatia ili kuhakikisha usalama wa mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Kwa upande mwingine watahiniwa hao walikuwa na stadi nzuri za uandishi wa majibu ya maswali ya insha. Hii inaonesha kuwa watahiniwa walijifunza vizuri mada ya Misingi ya Kufundishia Haiba na Michezo kwa sababu waliweza kufafanua vizuri mambo ya kuzingatia katika kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa hoja sahihi ya watahiniwa katika swali la 13 ni: *Kuzingatia kanuni na sheria za mchezo kwa mfano kuzingatia jinsia za wachezaji, kuzingatia ubora na matumizi sahihi ya vifaa vya michezo na mahali pa kuchezea/uwanja, kuzingatia afya za wachezaji mfano kuwepo kwa sanduku la huduma ya kwanza, kuzingatia umri wa wachezaji na aina ya*

*mchezo, kuhusianisha aina ya mchezo na umri wa mchezaji* na *wachezaji kufanya mazoezi ya mara kwa mara*. Watahiniwa waliwasilisha hoja zinazokidhi mahitaji ya swali. Hali hii ilimfanya waweze kufafanua hoja hizo kwa ufasaha. Kielelezo Na. 13. Ni sampuli ya kinaonesha majibu ya majibu swali la 13 vizuri.



13. Usalama: Ni hali ya kutokuwepo na hatari inayoweza kujitokeza katika kuhakikisha usalama wa Mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo. Yafuatayo ni Mambo ya kuzingatia ili kuhakikisha Usalama wa Wanafunzi.

Mahali pa kuchezea hii ina maana kwamba uwanja utakaotumika vikaguliwe kabla ya Mchezo kuanza ambapo watatoa uchafu wote ambao unaweza kuhatarisha afya za Watoto na kusababisha ajali zinazoweza kutokea wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo.

Vifaa vya kuchezea: hii ina maana kwamba vifaa vinavyotumika viandaliwe na kama vimeharibika viweze kufanyiwa Marekebisho ambapo Watoto wakianza kuvitumia vifaa hivyo wasipatwe na tatizo lolote ambalo linaweza kujitokeza ~~katika~~ wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la haiba na Michezo.

Afya ya Mchezaji: hii ina maana kwamba Mchezaji lazima awe na afya nzuri ambayo itamsaidia kuanza kucheza ambapo utakuta wanafunzi anakuwa anaumwa lakini ana lazimishwa kucheza ambayo inaweza kuleta hatari ambapo atakuwa na



3. Usalama wa Wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo.

Kufanya Mazoezi ya kupasha Mwili na kupoza Mwili kabla ya kuingia katika Mchezo ambapo Mwili hauwezi kupatwa na Magonjwa ya Mara kwa Mara ambapo atakuwa anaweza kuleta Matatizo kama ameingia uwanjani bila ya kufanya Mazoezi kwa hiyo ni lazima afanye Mazoezi ya kupasha mwili ili kuimarisha Usalama wa Wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo.

Chakula hii ina Maana kwamba ili kuimarisha usalama wakati wa Mchezo lazima Mchezaji apate chakula kitakachompa nguvu ya kuendelea kupambana katika Mchezo hivo ambapo itamsaidia Mchezaji kuwa na afya njema ambapo itamsaidia kuwa na Usalama wa Wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo.


Hata hivyo Wakizingatia Mambo hayo wanaweza kuwa na ufunzaji Mzuri wa vifaa wanavyotumia katika Mchezo Mbalimbali bila kuvipoteza au kuviharibu.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13


Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alifafanua hoja tano kuhusu mambo ya kuzingatia katika kuhakikisha usalama wa mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Kwa upande mwingine, asilimia 46 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani kutokana na baadhi yao kushindwa kutoa ufafanuzi wa kutosha wa hoja walizowasilisha. Aidha, baadhi ya watahiniwa walikosa maarifa na stadi za somo kuweza kufafanua mambo ya kuzingatia katika kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Aidha, asilimia 19 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata ufaulu hafifu kwa sababu miongoni mwao hawakuelewa matakwa ya swali. Wengine kati yao walikosa stadi za kujibu maswali ya insha. Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuwa wamechambua vizuri mada ya Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Haiba na michezo. Baadhi ya hoja za watahiniwa walioshindwa kuelewa matakwa ya swali ni pamoja na: *mwalimu kuwa na utayari katika kufundisha na kuwashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji, mwalimu kuhakikisha anatumia zana mbalimbali zinazomfirikirisha mwanafunzi, mwalimu awape wanafunzi uhuru wa kuuliza maswali na kusema changamoto zao, mwalimu anapaswa afundishe kwa ustadi kufikisha malengo mahsusi kwa walengwa*. Watahiniwa aliwasilisha hoja zisizokidhi mahitaji ya swali. Hali hii imemfanya wapate ufaulu hafifu katika swali la 13. Kilelezo Na. 13: 2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 13 vizuri.



13 Usalama wa wanafunzi, ni kitendo
mwalimu anapaswa kufahamu Idadi
ya wanafunzi wako katika mchakatu
tu mzima wa ufundishaji ili kufiki
malengo aliyokusudia kufikia.
Ushiriki wa wanafunzi wake
ti wa ujifunzaji, ni vema mwalim
u kujua ni jinsi gani wanafunzi
wake wanavyoshiriki katika suala
la zima la ufundishaji kwa muda
unaotakiwa wakati wa ujifunzaji
ili ni vema mwalimu kuhakikis
ha wanafunzi wako katika mcha
kato wa ufundishaji
Uwajibikaji katika kazi m
mbali mbali za shule, ni vema mw
afunzi kufanya usafi katika
maeneo yake ili kuhakikisha usafi
katika mazingira wanazozunguka
kujisimamia uwajibikaji ni jambo
muhimu ambayo mwanafunzi ana
takiwa kuwa nayo katika mcha
kato wa wa kufundishia na
kujifunzia
Kuwapatia wanafunzi mahitaji
mbali mbali, wanafunzi kupata ma
hitaji ni vema kwa sababu
ni mojawapo ya usalama wa wa
mwanafunzi ambao mwanafunzi an
apaswa kupata huduma hizo
mfano ni vema kuwapatia chanjo
mbali ambazo ni muhimu katika
huduma mbali mbali.



Uwepo wa chakula, Ni vema
mwanafunzi kupewa chakula wakati
wa mchakato mzima wa ufundi
shaji na ujifunzaji ili mwanafun
zi aweze kusoma vizuri katika
shughuli na kufanya kazi katika
mchakato mzima wa kufundishia
na kujifunzia.
Mazingira anamoishi, ni vema
mwalimu kutambua mwanafunzi
anaishi katika mazingira ambayo
ni mazuri pia ni bora kwa
afya yake ili kuweza kumudu
shughuli za ufundishaji na ujifunze
ji wa katika kuinua taaluma
yake.
Hivyo basi ni vema kujua
usalama wa mwanafunzi katika
mchakato wa ufundishaji na ujifu
nzaji katika somo la haiba na
michezo.


**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 13

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alishindwa kufafanua hoja tano za mambo ya kuzingatia katika kuhakikisha usalama wa mwanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

### 2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufasaha vipengele vitano vya andalio la somo na namna mwalimu anavyopaswa kuvitumia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kufafanua matumizi ya vipengele vya andalio la somo katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Jumla ya watahiniwa 1,111 sawa na asilimia 37.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa somo la Haiba na Michezo walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ni mzuri kwa sababu asilimia 98 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14*

Chati Na. 14: inaonesha kuwa asilimia 84.0 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, asilimia 14 walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na asilimia 2 walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Chati Na. 14; inaonesha kuwa asilimia 84 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu vizuri. Sababu za ufaulu mzuri ni kuwa baadhi ya watahiniwa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu vipengele vitano vya andalio la somo na jinsi vinavyotumika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Pia mada hii ni mada ambayo inafundishwa katika masomo mengi katika Vyuo vya Ualimu Ngazi ya Astashahada. Hali hii huwawezesha watahiniwa kuhawilisha maarifa na stadi kutoka masomo mengine kirahisi katika kujibu swali hili. Aidha, watahiniwa wote walifanya Mazoezi ya Ufundishaji kwa Vitendo (BTP) kwa miaka miwili mfululizo ya mafunzo yao. Mambo yote haya yaliwawezesha watahiniwa kufafanua kwa ufasaha vipengele vitano vya andalio la somo na ambavyo hutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo. Mfano wa majibu ya watahiniwa katika swali hili ni hii ifuatayo: *Umahiri mkuu, umahiri mahsusi, idadi ya vipindi, shughuli za ufundishaji na ujifunzaji, zana za kufundishia na kujifunzia, lengo kuu, mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana za kufundishia na kujifunzia na rejea.* Kielelezo Na. 14.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 14.


Katika kipengele cha utangulizi;
Katika kipengele cha utangulizi mwalimu anapaswa kutambulisha somo kwa kutafuta maarifa ya awali kutoka kwa wanafunzi. Kwa mfano mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali yanayohusiana na somo husika.

Kipengele cha kujenga umahiri; Katika kipengele cha kujenga umahiri mwalimu anapaswa kuwashirikisha wanafunzi kujenga umahiri kwa kujadili pamoja na wanafunzi kutumia mada husika. Kwa mfano mwalimu anaweza kutoa kazi za majadiliano katika vikundi kisha kupitia katika kila kundi kwa majadiliano.

Kipengele cha kuimarisha umahiri; Katika kipengele hiki mwalimu anaweza kuwauliza maswali wanafunzi mmoja mmoja kuhusiana na umahiri uliojengwa. Kwa mfano mwalimu anaweza kutoa swali kwa kila mwanafunzi akalijibu katika daftari lake.

Kipengele cha hitimisho. Katika kipengele cha hitimisho mwalimu anaweza kutoa kazi ya kufanya ambayo kila mwanafunzi ataifanya katika daftari lake. Kwa mfano mwalimu anaweza kutoa kazi ya maswali kumi na baada ya hapo akaisahihisha.

Kipengele cha tathmini ya somo: Katika kipengele cha tathmini ya somo, mwalimu anapaswa kutathmini hali ya somo kuanzia utangulizi hadi hitimisho na kubaini mafanikio au mapungufu kama yapo na kupendekeza namna ya kuyatatua katika vipindi vijavyo. Kwa kutoa mazoezi ya ziada kwa ambao hawajaelewa.


Kipengele cha tathmini ya somo
Katika kipengele cha tathmini ya somo, mwalimu anapaswa kutafakari hali ya somo kuanzia utangulizi hadi hitimisho na kubaini mafanikio au mapungufu katika somo ya kupendekeza namna ya kuliboresha zaidi. Kwa kutoa mazoezi ya ziada kwa ambao hawajaelewa.

**Kielelezo Na. 14.1:** *Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 14*

Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa aliweza kufafanua vizuri vipengele vitano vya andalio la somo na namna mwalimu anavyopaswa kuvitumia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Kwa upande mwingine, asilimia 14 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani. Hii ni kutokana na baadhi ya watahiniwa kuacha kutoa utangulizi wa swali na kuanza kujibu swali moja kwa moja. Aidha, baadhi ya watahiniwa waliweza kuwasilisha na kufafanua hoja chache kuliko matakwa ya swali.

Watahiniwa 26 (2%) walikuwa na ufaulu hafifu kwa sababu baadhi yao walikuwa na uelewa hafifu wa maarifa na stadi kuhusu maandalio ya masomo ya Haiba na Michezo. Hali hii ina onesha kuwa baadhi ya watahiniwa hawakuchambua vizuri na kuielewa mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo, hususan katika kipengele cha maandalio ya somo. Baadhi ya hoja za watahiniwa zilikuwa ni: *Ili kumsaidia kutumia muda wake vizuri wakati wa ufundishaji, kutimiza malengo mahsusi ya somo lake, kumsaidia mwanafunzi kuelewa kwa haraka somo au mada, kuwawezesha wanafunzi kushiriki vizuri wakati wa kujifunza na kuweza kutumia zana zake na mbinu zake alizoziandaa.*

Udhaifu wa hoja hizi ulisababisha watahiniwa wapate alama na ufaulu hafifu katika swali hili. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 14 vizuri.

14. Andalio la Somo. Ni mpango mfupi / maandalizi ya mwalimu aliyoandaa kufu. kabla ya kuingia darasani kufundisha. Mfano, Mada, Muda atakaotumia, Zana atakazotumia kufundishia

ii Namna mwalimu anavyopaswa kutumia Vipengele vya andalio la somo wakati wa Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo ni

Kuzingatia umahiri mkuu. Hapa Mwalimu anapaswa kuzingatia kwa makini ili asitoke nje ya lengo kuu.

Kuhusanisha umahiri mahususi. uliopo kwenye andalio na an: kitu anacho-fundisha darasani, Hivyo basi mwalimu Anapaswa kuzingatia aliyoandaa/andika kwenye andalio la somo,

Kuhusanisha Zana na mada anayofundi-shaj Hapa mwalimu lazima ahusanishe Zana alizoandaa kufundishia na kujifunzia Somo la haiba na michezo.

Kujenga umahiri mahususi. kulingana Na kipengele kwenye andalio mwalimu anatakiwa kujenga umahiri mahususi wakati wa kujifunza na kufundisha Somo la Haiba na michezo!

Kuimarisha shughuli mahususi. Mwalimu anapaswa kuimarisha Shughuli Mahususi kwa kurekebisha makosa.

Hivyo basi, Mwalimu anapaswa kutoa kutoa maswali ya upimaji baada ya kumaliza swala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na michezo.

**Kielelezo Na. 14.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 14


Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alishindwa kueleza kwa ufasaha namna ambayo mwalimu anapaswa kutumia vipengele vitano vya andalio la somo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

### 2.2.5 Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa afafanue vipengele vitano vya Azimio la Kazi ambavyo hutumika wakati wa maandalizi ya andalio la somo la Haiba na Michezo. Lengo la swali hili lilikuwa kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuweka bayana vipengele vitano vya maazimio ya kazi ambavyo

hutumika wakati wa kuandaa maandalio ya masomo ya somo la Haiba na Michezo.

Watahiniwa 2,156 sawa na asilimia 73.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa somo la Haiba na Michezo walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa hili swali ni mzuri kwa sababu asilimia 99.3ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 15 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa waliojibu swali la 15.





**Chati Na. 15:** Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 15

Chati Na. 15 inaonesha kuwa watahiniwa asilimia 82.2 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, asilimia 17.1 walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na asilimia 0.6 walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 82.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri. Sababu za watahiniwa hao kufaulu kwa kiwango hicho ni kwa sababu wengi wao, mbali na kuelewa matakwa ya swali, walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo, hususani katika vipengele vya Azimio la Kazi na Andalio ya somo. Kutokana na uelewa huo, watahiniwa wengi waliweza kufafanua kwa ufasaha vipengele vya Azimio la Kazi ambavyo hutumika wakati wa maandalizi ya Andalio la somo la Haiba na Michezo. Mfano wa majibu sahihi ya watahiniwa katika

swali hili ni: *Ujuzi, mada kuu, mada ndogo, idadi ya vipindi, mbinu za kufundishia na kujifunzia, vifaa au zana za kufundishia na kujifunzia, rejea, upimaji, maoni* kwa mtaala wa ujuzi na *Umahiri mkuu, umahiri mahsusi, vitendo vya ufundishaji, vitendo vya ujifunzaji, idadi ya vipindi, zana/vifaa ya kufundishia na kujifunzia, zana za upimaji na rejea.* Watahiniwa waliwasilisha hoja sahihi kwa mahitaji ya swali la 15. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 15.



15. Azimio la kazi; Ni mpango wa Muda Mrefu anaoweza kujiwekea Mwalimu katika Ufundishaji wake ambapo ataweza kuandika katika kipindi cha Miezi Sita au Mwaka Mzima kwa Vipengele ambavyo hutumika katika kuandaa Andalio la somo la Haiba na Michezo.

Vifuatavyo ni Vipengele vya Azimio la kazi ambavyo hutumika wakati wa Maandalizi ya Andalio la somo la Haiba na Michezo.

Umahiri Mkuu; Ni lengo kuu ambalo ataweza kulitumia mwalimu kufundishia Mwalimu ndani ya Muda Mrefu au mada ambayo mwalimu anatakiwa kufundisha darasani anapotaka kuandalia somo lazima kuanza kuita mbulisha Umahiri Mkuu atakaokuwa anaupata.

Umahiri Mahususi; Lengo mahususi ambalo mwalimu atalifundisha kwa muda Mfupi kulingana na Umahiri Mkuu utakavyo kuwa Unavyona au ni vipengele vidogo vidogo vili vyopo ndani ya Umahiri Mkuu ambapo atatakiwa Mwalimu kuvipitia katika Ufundishaji wake.

Zana za kufundishia na kujifunzia; Pia katika azimio mwalimu ataweza kuangalia zana ambazo zitaweza kumuongoza katika Ufundishaji na Ujifunzaji kwa mwalimu na mwanafunzi ili kuweza kulifikia lengo alilotaka kujiwekea katika Mtakatak wake wa Ufundishaji.

Idadi ya Vipindi; Pia tunapoweza kuandalia tunaweza kuangalia idadi ya Vipindi katika azimio la kazi kulingana na Umahiri mahususi ambao tunatakiwa kufundisha kwa sababu kila Umahiri Mahususi unakuwa na idadi ya Vipindi ambavyo hufundishwa kulingana na Uzito wa Umahiri huwo.

Shughuli za Ufundishaji; Mwalimu ataweza kuangalia Shughuli ambazo anatakiwa kufanya mwalimu katika Ufundishaji wake ili aweze kuziweka katika andalio kabla ya kwenda kuingia darasani kufundisha ambazo zitaweza kumuongoza katika kulifikia lengo.


Hivyo Vipengele vya Azimio la kazi huweza kutumika katika kuandaa Andalio la somo kwa Mwalimu ambapo ataweza kuandaa somo kama azimio litakavyokuwa lina muongoza ili kuweza kulifikia lengo la Somo la haiba na Michezo.


**Kielelezo Na. 15.1** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 15

Katika Kielelezo Na. 15.1, mtahiniwa amewasilisha hoja zinazokidhi mahitaji ya swali. Hali hii imemfanya aweze kubainisha hoja hizo kwa ufasaha.

Kwa upande mwingine, asilimia 17.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani. Hali hii ilisababishwa na baadhi ya watahiniwa kutoa utangulizi na hitimisho ambayo haiendani na swali. Mbali na hayo, miongoni mwa watahiniwa walitoa hoja chache tofauti na mahitaji ya swali. Aidha, watahiniwa wengine walikosa ufafanuzi wa kutosha kuthibitisha hoja zao. Pia watahiniwa wengi walitoa hoja chache tofauti na matakwa ya swali. Mbali na hayo, baadhi ya watahiniwa walirudia hoja moja kwa kutumia maneno mengine. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi lakini bila ufafanuzi.

Aidha, watahiniwa wachache (0.6%) walipata ufaulu hafifu. Sababu za kupata ufaulu hafifu ni kuwa baadhi yao hawakuelewa swali. Sababu nyingine ni baadhi yao kukosa stadi bora za kujibu maswali ya insha. Hali hii ilisababisha watahiniwa hao kutoa maelezo mafupi sana katika kufafanua hoja zao. Hii inadhirisha kuwa walifanya maandalizi mabovu katika kujifunza mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo hili, hususan katika vipengele vya Azimio la Kazi na Andalio la somo. Mfano wa majibu duni ambayo watahiniwa waliwasilisha ni: *Utangulizi, maarifa mapya, kujenga maarifa, kukazia maarifa na hitimisho.* Watahiniwa wamewasilisha hoja zisizokidhi mahitaji ya swali. Majibu waliyotoa ni hatua za somo ndani ya maandalio ya masomo. Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 15.


15 Katika maandalizi ya ufundishaji inafaa zaidi kuwa na vifaa mbalimbali vitakavyo kusaidia katika maandalizi yako ya ufundishaji ninyi na wewe na azimio la kazi, andalio la somo, vitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu ambayo vitakufanya uwe mahiri zaidi katika ufundishaji wako.
Vifuatavyo ni vipengele vya azimio la kazi ambavyo hutumika wakati wa maandalizi ya andalio la somo:



Hatua za ufundishaji; katika kipengele hiki huwa tunaangalia mwalimu anafundisha katika vitendo gani maalum kwa katika utangulizi, kujenga umahiri, kuimarisha umahiri na kuhitimisha somo kwa kutoa zoezi.

Muda wa ufundishaji; katika kipengele hiki huwa tunaangalia ni muda gani utakaotumika kufundisha umahiri fulani ulioandikwa katika somo na kwa kila hatua huwa na dakika zake za kufundisha na kuimarisha zaidi na kuweza kufikia malengo.

Vitendo vya ufundishaji; katika vitendo hivi hapa mtendaji ni mwalimu huwa kutoa muongozo kwa wanafunzi kisha kuwafafanulia mambo mbalimbali na hatimae kuelewa kile kinachofundishwa.

Vitendo vya ujifunzaji; hiki pia ni kipengele moja wapo ambapo mtendaji

15 mtendaji kile anacho elekezwa na mwalimu hatimae hupelekea kujijengea maarifa mapya na kupata ujuzi zaidi.

Viashiria vya ujifunzaji; katika viashiria hivi hapa mtendaji ni mwanafunzi kwani huonesha mwitikio wa mwanafunzi juu ya jambo analoletewa kwa kuwa analimudu au hakumudu, pia katika viashiria vya ufundishaji huonesha mwitikio wa wanafunzi katika ujuzi mpya alioupata.

Hivyo basi ni baadhi ya vipengele vya azimio la kazi vinavyotumika katika mchakato mzima wa ufundishaji na kuleta mafanikio makubwa zaidi.


**Kielelezo Na. 15.2** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 15

Katika Kielelezo Na. 15.2; mtahiniwa aliwasilisha hoja ambazo hazikidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa amewasilisha vipengele vya Andalio la Somo badala ya vipengele vya Azimio la Kazi.

### 2.2.6 Swali la 16: Upimaji na tathmini katika somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa athibitishe kwa hoja tano kauli kwamba "Shajara ni mojawapo ya nyaraka muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo". Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutathmni umuhimu wa shajala ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Jumla ya watahiniwa 2,536 (100%) walijibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa swali hili ni mzuri kwa sababu asilimia 99.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 16 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 16.




**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa asilimia 61.2 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, asilimia 38.2 walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na asilimia 6.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Chati Na. 16 inaonesha kuwa asilimia 61.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri. Sababu za ufaulu kuwa mzuri ni kuwa baadhi ya watahiniwa walitambua vema mahitaji ya swali. Hali hii iliwawezesha kuthibitisha kwa hoja tano umuhimu wa shajara katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Hii inadhihirisha kuwa baadhi ya watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha wa mada ya Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji ambapo kipengele cha shajara ya somo hufundishwa. Hivyo, watahiniwa wengi waliweza kueleza kwa ufasaha umuhimu wa shajara ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa baadhi ya hoja za watahiniwa ni: *Shajara ya somo humsaidia mwalimu mkuu kujua maendeleo ya ufundishaji wa somo na kutoa maoni juu ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wake, husaidia wakati wa makabidhiano ya somo inapotokea dharura kwa mwalimu kwani shajara huonesha mada zilizofundishwa, huwasaidia wathibiti ubora kubaini kama ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi ulienda vizuri au la hutumiwa na watafiti wa kielemu kujua maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni.* Watahiniwa hao waliwasilisha hoja zilizokidhi mahitaji ya swali. Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali la 16 kwa usahihi.

16. Shajara ni daftari ambalo huwa na kumbukumbu ambazo mwalimu amezi andika dhana aliyozifundisha na tarehe ambazo amefundisha mambo hayo.


Ni kweli kwamba shajara ni moja kati ya nyaraka muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji somo la Haiba na michezo. Nathibitisha kauli hii kwa kutoa umuhimu wa shajara katika shule zima la ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Shajara humsaidia mwalimu kujua vitu alivyovifundisha; yaani humsaidia mwalimu kuepuka kurudia tena vitu ambavyo tayari amevifundisha. Kwa kuwa shajara la somo huonyesha dhana iliyofundishwa tarehe ambayo amefundisha mambo hayo, wiki na mwezi pia hivyo kutokana na kumbukumbu hiyo humsaidia mwalimu kuepuka kurudia vitu alivyovifundisha,

Shajara humsaidia mwalimu katika uandaaji wa maazimio na utungaji wa mitihani pia kwa kuwa Shajara shajara huonyesha mbambo yote ambayo mwalimu amefundisha hivyo humsaidia katika kuandaa mitihani mbalimbali. Kwa hiyo Shajara hutumika katika maandalizi ya somo kuandaa mtihani

Shajara humsaidia mwalimu mwingine kupokea somo endapo mwalimu wa somo husika atapata dharura, pia hii ni mojawapo ya matumizi ya shajara ya somo humsaidia mwalimu mgeni kuendelea kufundisha somo endapo mwalimu wa somo atapata dharura

Shajara humsaidia mwalimu mkuu kujua maendeleo ya mwalimu katika ufundishaji pia huu ni mojawapo wa umuhimu wa shajara ya somo hapa mwalimu mkuu atajua kama mwalimu wa somo la Haiba na michezo anamaendeleo gani katika suala zima la ufundishaji. Kutokana na kuwa shajara huandaliwa kila baada ya wiki vitu ambavyo mwalimu amevifundisha kwa wiki nzima hivyo lazima ziende kusainiwa kwa mwalimu mkuu hivyo hapo ndipo mwalimu mkuu huangalia vipengele alivyovifundisha na kutoa mapendekezo endapo mwalimu wa somo atakuwa tofauti.



Shajara huwasaidia wadhibiti ubora kujua maendeleo ya ufundishaji kwa mwalimu, pia endapo wadhibiti ubora watapenda shuleni kukagua walimu maendeleo yao hivyo watafanya tathmini vyote walivyokua wanatumia katika ufundishaji na shajara likiwemo. Hivyo endapo wadhibiti ubora watakabiziwa shajara wataona vitu ambavyo mwalimu kufundisha na kutoa mapendekezo yao hivyo watajua kwa je mwalimu wa somo anamaendeleo gani katika suala la ufundishaji.

Kwaujumla shajara ya somo ina umuhimu wake katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji.


**Kielelezo Na. 16.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 16

Katika Kielelezo Na. 16.1, mtahiniwa aliweza kuthibitisha umuhimu wa shajara ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

Kwa upande mwingine, asilimia 32 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata ufaulu wa wastani. Hali hii ilisababishwa na baadhi ya watahiniwa kutoa hoja chache tofauti na mahitaji ya swali. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi lakini bila uthibitisho wa kutosha. Mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *'...kumsaidia mwalimu kutunza kumbukumbu za ufundishaji; Shajara huweza kumsaidia mwalimu katika utunzaji wa kumbukumbu za ufundishaji na ujifunzaji'.* Aya nyingine anaendelea na kusema, '*Kumsaidia mwalimu kutorudia somo. Pia shajara humsaidia Mwalimu kutorudia kufundisha somo kwa kuangalia kumbukumbu zake za ufundishaji'.* Huu ni uandishi mbovu wa insha.

Aidha, watahiniwa wachache (6%) walipata ufaulu hafifu kwa sababu walikosa maarifa ya kutosha kuhusiana na umuhimu wa shajara ya somo la Haiba na Michezo. Watahiniwa wengine walikosa stadi za kujibu maswali ya insha. Matokeo yake waliwasilisha hoja ambazo hazikukidhi matakwa ya swali na kushindwa kuzitetea. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa hawakutilia maanani ufundishaji na ujazaji

wa shajara ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji vyuoni. Hali hiyo iliwafanya baadhi ya watahiniwa kushindwa kuthibitisha umuhimu wa shajara ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa majibu yasiyosahihi ya watahiniwa waliojibu swali hili ni: *Shajara ya somo hurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa sababu mwalimu atakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kile atakachofundisha, humsaidia mwalimu wa somo kutambua changamoto wanazokutana nazo wanafunzi darasani na kuzitatua, humsaidia mwalimu kujiongezea maarifa mbalimbali, humsaidia mwalimu kuboresha njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji na humwongoza mwalimu kufundisha kuendana na mtiririko mzuri wa mada.* Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mtahiniwa katka swali la 16.


16. Shajala ni nyaraka ambayo inaandali
wa na mwalimu Kila baada ya ku
maliza wiki ili kuweza kujua ka
ma Wanafunzi wamewera kuelewa vi
zuri juu ya kile ambacho umekufundi
sha. Ufuatao ni umuhimu wa shajala
Katika mchakato wa ufundishaji na ujifu
nzaji wa somo la haiba na michezo.
Inamsaidia mwalimu mgeni kuende
lea kufundisha pale ambapo mwalim
u muhusika wa somo hata kuep
o atawera kujua wapi aendelee kuto
kana na shajala la somo.

6. Inamsaidia mwalimu wakati wa ut
ungaji wa mtihani; pale ambapo mwalim
utaandaa shajala la somo itakusaidia
wakati wa kutunga mtihani kujua
ni mada zipi ambazo umekwisha fu
ndisha.
Inamsaidia mwalimu kujua mada
ambazo amekwisha kufundisha. endapo
mwalimu ukuwa unaandika shajala
la somo itakusaidia kujua ni mada
zipi ambazo tayari umeshafundish
kutokana na kumbukumbu zinazo
Inamsaidia mwalimu kujua mbin
u gani aboreshe wakati wa ufundi
shaji kwa sababu kunakuwa na
maoni ya mtaaluma pamoja na ya
mkuu wa shule hivyo ni lazima
ujue ni mbinu gani unatakiwa uboreshe
Inamsaidia mwalimu kuweza kuwatu
mbua wanafunzi wenye changamoto au
matatizo mbalimbali na kuweza kuwa
tafutia ufumbuzi wake kutokana na
maoni yanayopatikana katika shajala.
Hivyo basi shajala la somo ni
la muhimu sana kwa mwalimu
kwa sababu huweza kujua na ku
boresha mbinu za ufundishaji w
ake ili wanafunzi waweze kuelewa.

**Kielelezo Na. 16.2:** Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika Swali la 16

Katika Kilelelezo Na. 16.2 mtahiniwa alishindwa kuthibitisha umuhimu wa shajara ya somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

Kiwango cha ufaulu katika mada tano zilizotahiniwa mwaka 2021 kilikuwa kizuri. Katika mada hizo watahiniwa walifanya vizuri katika mada nne (4) ambazo ni; *Upimaji na tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Hiaba na Michezo* (99.4%), *Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia* (95.97%), *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo* (92.88%) na *Maandalizi ya Ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo* (90.95%). Ufaulu wa kiwango kizuri katika mada nne umetokana na sababu mbali mbali kama vile watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na umahiri wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, uelewa mzuri wa maswali na mtiririko mzuri wa hoja ambao ulikidhi vigezo vya uandishi wa insha. Aidha watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani katika mada ya; *zana za kufundishia na kujifunzia* (67.95%).

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Ufaulu wa watahiniwa wa ualimu Daraja A katika somo la Haiba na Michezo ulikuwa ni mzuri katika mada zote. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2021 katika mada zote kilikuwa ni asilimia mia moja (100%). Ufaulu huu umetokana na watahiniwa kuelewa matakwa ya maswali, kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na kutoa ufafanuzi unaotosheleza.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuendeleza kiwango kizuri cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Haiba na Michezo katika siku zijazo inapendekezwa kuwa:

(i) Wanachuo waendelee kufanya mazoezi ya kutosha ya Ufundishaji Kiduchu (Micro-teaching Practices) na Ufundishaji Vipindi Shuleni (Single Lesson Teaching Practice) ili kujenga uwezo wa kuelewa mada za Haiba na Michezo kwa kina.

(ii) Wanachuo wasome kwa kina mada zote kama zilivyoainishwa kwenye muhtasari wa somo la Haiba na Michezo ili kupata maarifa, stadi na mwelekeo sahihi katika mada hizo na somo la Haiba na Michezo kwa ujumla.

*Kiambatisho A*

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA MWAKA 2021**

| Na. | Mada | Namba ya swali | Asilimia ya ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ufaulu katika kila swali (%) | Wastani wa ufaulu katika kila mada (%) | |
| *1* | Upimaji na tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Hiaba na Michezo | 1 | 99.4 | 99.4 | Vizuri |
| *2* | Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 5 | 92 | 95.97 | Vizuri |
| | | 10 | 96 | | |
| | | 11 | 99.9 | | |
| *3* | Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo | 3 | 6.5 | 92.88 | Vizuri |
| | | 6 | 97 | | |
| | | 12 | 97 | | |
| | | 13 | 81 | | |
| *4* | Maandalizi ya Ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo | 2 | 85 | 90.95 | Vizuri |
| | | 4 | 82 | | |
| | | 8 | 82 | | |
| | | 14 | 98 | | |
| | | 15 | 99.3 | | |
| | | 16 | 99.4 | | |
| *5* | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 7 | 44.9 | 67.95 | Wastani |
| | | 9 | 91 | | |